KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 17, Issue 2

13th Muharram 1433

9th Dec, 2011

YALIYOMO

SIJDA KWA AJILI YA KUSAHAU NDANI YA SWALA

SUJOOD AS-SAHW 1 - 4

Na: Sheikh Muhammad ibn Saaleh al-'Uthaymeen (رحمه الله)

UTANGULIZI:

Sifa zote njema ni zenye kumthubutukia Allaah, Mola wa viumbe vyote, Tunamuomba Yeye Amsifu na Kumbariki Mtume wetu Muhammad (صلى الله عليه وسلم), ambae aliye-ufikiliza ujumbe, na vilevile wafuasi wake wa kweli, Maswahaba zake, na wote walowafuata wao kwa wema hadi siku ya malipo. Mwanzo kabisa:

Kwa hakika watu wengi hawajui kuhusu hukmu inayohusiana na Sujood as-Sahw (kusujudu kwa ajili ya kusahau) ndani ya swala. Kuna wale ambao wasoitekeleza sujood as-Sahw mahali ambapo wanapowajibika kuitekeleza; na wengine huitekeleza sijda hiyo mahali ambapo si sawa kwao wao kuitekeleza; wengine huitekeleza (Sujood as-Sahw) kabla ya salaam (maamkuzi mwishoni mwa swala) hata kama iliwapasa kufanya hivyo baada ya salaam; wengine huitekeleza baada ya salaam hata kama iliwapasa kufanya hivyo kabla ya salaam. Kwahivyo ni muhimu sana kuzijua hukmu zake, hususan kwa ma-Imaam wenye kuwaongoza watu kwenye swala zao, haliyakuwa wao wamechukua jukumu la kuandama matekelezo yaliyo sawa kwenye swala zao, na kuwaongozea Waislamu kwayo. Ndio mimi nikaonelea ni bora kuwaletea ndugu zangu baadhi ya hukmu zinazohusiana na mas-ala haya, nikitarajia yakwamba Allaah, Alie juu zaidi, Atalisababisha jambo hili kuwa ni lenye manufaa kwa waja Wake waumini. Mimi nasema, nikitarajia usaidizi kutoka kwa Allaah, Alie juu zaidi, na kumuomba Yeye uongofu na Atupe sisi yale yaliyo ya sawa;

SIJDAT AS-SAHW ni: Sijda mbili ambazo zinazotekelezwa na mwenye kuswali kwa ajili ya kufidia/kurekebisha makosa yatokeayo akiwa ndani ya swala kutokana na kusahau (Sahw). Kuitekeleza sijda hii kunasababishwa na mambo matatu: Kuzidisha kitu **(az-Ziyaadah)**, Kuwacha kitu **(an-Naqs)** na kuwa na shaka **(ash-Shakk).**

(I) KUZIDISHA KITU (*az-Ziyaadah*)

Ikiwa mwenye kuswali ataongeza kitu katika swala yake kwa makusudi kama vile kisimamo, kikao, rukoo' au sijda, basi itakuwa swala yake ni baatil (haifai). Hatahivyo, iwapo atafanya nyongeza yoyote kwa kughafilika na asiikumbuke nyongeza hiyo mpaka ikamilikapo, basi hapana chochote chenye kumpasa yeye isipokuwa sujood as-Sahw, na swala yake itakuwa sawa. Na ikiwa atakumbuka (nyongeza hiyo) haliyakuwa yukatika hiyo nyongeza, atawajibika kuiwacha nyongeza hiyo na vilevile aitekeleze sujood as-Sahw (yaani: mwishoni mwa swala), na swala yake itakuwa sawa. Kwa mfano, ikiwa mtu ameswali swala ya adhuhuri raka'ah tano, na asikumbuke yakwamba amefanya nyongeza mpaka alipokuwa kwenye tashah-hud. Itampasa mtu huyu kuitimiza tashah-hud, na atoe maamkuzi (atoe salaam), kisha asujudu kwa ajili ya kusahau, kisha atoe tena salaam (kwa mara ya pili). Hatahivyo, iwapo hatokumbuka nyongeza hiyo mpaka baada ya kutoa salaam, basi itambidi asujudu kwa ajili ya kusahau na kisha atoe tena salaam. Ushahidi wa jambo hili ni hadeeth ya 'Abdullaah ibn Mas'ood (رضي الله عنه) aliesema yakwamba, "Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliswali swala ya adhuhuri raka'ah tano, na mtu mmoja akasema, 'Kumefanywa nyongeza yoyote katika swala?' Nae Mtume (صلى الله عليه وسلم) akajibu, 'Na ni kwanini iwe hivyo?', Wakasema, 'Wewe umeswali (raka'ah) tano'. Kwahivyo akatekeleza sijda mbili baada ya kutoa salaam..." na katika riwaya nyengine (kunapatikana maneno yasemayo), "... na akageuza miguu yake na kuelekea Qiblah, na akatekeleza sijda mbili, kisha akatoa salaam." Ilipokewa na kikosi kizima.

KUTOA SALAAM KABLA YA SWALA

KUKAMILIKA

Kutoa salaam kabla ya swala kukamilika ni miongoni mwa nyongeza katika swala. Kwahivyo yeyote mwenye kutoa salaam kabla ya swala kukamilika kwa kukusudia, basi swala yake ni baatil (haifai). Hatahivyo, iwapo limefanywa jambo hilo kutokana na kusahau, na mtu akakumbuka baada ya kupita muda mrefu, itambidi mtu huyo airudie tena swala yake. Ikiwa amekumbuka kwa muda mchache baadae kama vile dakika mbili au tatu, basi itambidi aikamilishe swala yake pamoja na kutoa salaam, na kisha atoe tena salaam (mara ya pili). Ushahidi wa jambo hili ni hadeeth ya Abu Hurairah (رضي الله عنه) aliesema yakwamba; Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwaongoza kwenye swala ya adhuhuri au 'Asr akatoa salaam baada ya raka'ah mbili. Kisha akaondoka kwa upesi kwa kupitia kwenye mlango mmoja wa msikiti, na watu wakawa wanasema yakwamba swala imepunguzwa. Palepale, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasimama kwenye kipande cha gogo kilichokuwa ndani ya msikiti, amejitegemeza hapo, akionekana kama ameudhika. Akasimama mtu mmoja akasema, "Ewe Mtume wa Allaah, umeghafilika ama swala imepunguzwa?". Basi akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم), "Mimi sikughafilika wala swala haikupunguzwa." Yule mtu nae akasema, "Na'am kwa hakika umeghafilika." Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawauliza Maswahaba zake, "Je, anayoyasema mtu huyu ni ya kweli?" wakasema, "Na'am". Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasongea mbele na kuswali kilichopungua katika swala yake, akatoa salaam, kisha akasujudu mara mbili na mwisho akatoa salaam. Wakaafikiana juu ya jambo hilo. [1]

Na iwapo Imaam ametoa salaam kabla ya swala yake kukamilika na

kulikuwa na baadhi ya wafuasi walokosa sehemu ya swala na wakawa wamesimama kukamilisha yaliyowapita, na kisha Imaam akakumbuka yakwamba kwenye swala yake kulikuwa na upungufu fulani ulompasa kuukamilisha, basi akasimama yeye kukamilisha jambo hilo - katika hali hii wale wafuasi ambao tayari wameshasimama ili kukamilisha yaliyowapita wana khiyari baina ya kuendelea kukamilisha yaliyowapita na hatimae kumalizia kwa kutekeleza sijda ya kusahau na baina ya kurudi na kumfuata Imaam - na anapotekeleza salaam katika kukamilisha yale yalowapita - na kisha kusujudu kwa ajili ya kughafilika baada ya kutoa salaam na hili ndilo jambo lilosawa zaidi na ni jambo la busara.

(II) KUWACHA KITU (*Naqs*)

Kuwacha Nguzo (Arkaan) - Mtu akiacha nguzo (Rukn) katika swala yake, kama takbeer ya mwanzo (Takbeeratul Ihraam) basi atakuwa hana swala mtu huyu, emma aliiwacha kwa kukusudia au kwa kughafilika kwa sababu swala yake haijaanza. Ikiwa ni jambo lolote jengine lisilokuwa Takbeer ya mwanzo, basi hapo ikiwa ameliacha jambo hilo kwa kukusudia swala yake inakuwa ni baatil. Hatahivyo, iwapo ataliwacha jambo hilo kwa kughafilika, kisha akaendelea mpaka akafika tena mahali hapo kwenye raka'ah nyengine, basi ataibeua (kuwachana nayo) ile raka'ah ambayo ndani yake alikisahau kile kitendo na hiyo raka'ah nyengine ikachukuwa nafasi hiyo badala ya ile ya kwanza. Na ikiwa hajafika mahala pale kwenye raka'ah iliyofuata, basi atawajibika arudi katika ile nguzo aloikosa ili aitekeleze na kila kifuatacho baada yake. Katika hali zote mbili hizo, atawajibika kutekeleza sijda ya kusahau baada ya kutoa salaam. Mfano wake (jambo hili) ni mtu alokatika hali ya raka'ah ya kwanza na akasahau sijda ya pili, lakini akakumbuka jambo hilo alipokuwa katika kikao baina ya sijda mbili kwenye raka'ah ya pili. Basi itambidi aibeue raka'ah ya kwanza na raka'ah ya pili ichukue nafasi hiyo kuwa ndiyo raka'ah yake ya kwanza na akamilishe swala yake kwa makadirio hayo. Kisha na atoe salaam, asujudu sujood as-Sahw, na kisha atoe salaam. Mfano wa ziada (ni ule wa) ikiwa mtu amesahau sijda ya pili na kikao cha kabla yake kwenye raka'ah ya kwanza. Lakini akakumbuka jambo hilo baada ya kusimama wima kutoka kwenye rukoo' katika raka'ah ya pili. Itambidi arudi katika kikao na asujudu, na kisha aikamilishe swala yake kutokea hapo. Kisha na atoe salaam, asujudu sujood as-Sahw, na hatimae atoe salaam.

KUWACHA YALIYO WAAJIB (WAAJIBAAT)

Iwapo mwenye kuswali ameacha jambo la waajib kutoka katika mambo ya waajib juu ya mwenye kuswali kwa kukusudia, itakuwa swala yake baatil (haifai). Hatahivyo, ikiwa amefanya hivyo kutokana na kughafilika, na akakumbuka kabla hajaendelea mbele na swala yake, basi na atekeleze jambo hilo, na wala haitompasa chochote cha ziada. Ikiwa atakumbuka baada yakwamba ashaendelea kutoka mahali pale kwenye swala yake, lakini akawa hajafika kwenye nguzo inayoifuata, kisha atairudia na aitekeleze (nguzo hiyo). Kisha ataikamilisha swala yake na atoe salaam, asujudu sujood as-Sahw, na atoe salaam. Hatahivyo, akakumbuka baada ya kuifikia nguzo inayoifuata, basi itafutiliwa mbali, kwahivyo hatoirudia tena lakini na aiendeleze swala yake kisha asujudu sujood as-Sahw **kabla** ya kutoa salaam.

Kwa mfano, ainukapo mtu kutoka katika sijda ya pili ya raka'ah ya pili ili asimame kwa raka'ah ya tatu na kusahau tashah-hud yakwanza. Lakini akakumbuka kabla hata hajasimama wima, basi na abakie kwenye hali ya kukaa, akae kwa tashah-hud na kisha akamilishe swala yake - na wala haitompasa chochote cha ziada. Hatahivyo, akikumbuka baada ya kuanza kusimama lakini kabla ya kusimama wima, basi na arudi kwenye kikao chake na atekeleze tashah-hud. Kisha na akamilishe swala yake na atoe salaam, asujudu sujood as-Sahw, na atoe salaam.

Akikumbuka baada ya kusimama wima, basi tashah-hud itafutiliwa mbali kwake, hatoirudia. Bali ataendelea na akamilishe swala yake, na asujudu (sujood as-Sahw) **kabla** ya kutoa salaam.

(III) KUWA NA SHAKA (*Shakk*)

Kuwa na shakk ni kutokuwa na hakika kuhusu jambo lilotokea baina ya mambo mawili; na shaka haina uzito wowote kwenye mas-ala ya ibaadah katika mambo matatu;

(i) Huku ni kughurika, kutokuwa na ukweli wowote, kama vile mnong'ono wa Shetani.

(ii) Shaka inapomjia mtu sana kiasi cha kwamba kila afanyapo ibaadah ya aina yoyote, huandamana na shaka.

(iii) Itakapomjia shaka baada ya kukamilisha kitendo cha ibaadah basi huwa haina uzito wowote, maadamu hana uhakika wa shaka hiyo, basi itampasa atekeleze lile alinahakika nalo.

Mfano wa haya ni iwapo mtu ameswali swala ya adhuhuri, na baada ya kuikamilisha swala yake akawa na shaka emma ameswali rakaa'ah tatu au nne. Kisha shaka isimjie mpaka awe na uhakika yakwamba yeye ameswali rakaa'ah tatu tu, na katika hali hii itampasa aikamilishe swala yake likimtokea jambo hilo muda mchache baadae, kisha atoe salaamu, asujudu (sujood as-Sahw) na hatimae atoe tena salamu. Hatahivyo, ikiwa hatokumbuka mpaka muda mrefu ukapita, basi itambidi airudie swala yote kamili.

Amma kuhusu shaka zisokuwa katika hali hizi tatu, basi zitakuwa ni zenye kuhesabiwa. Shaka katika swala ni aina mbili:

(i) Katika fahamu zake, jambo moja litakuwa na uzito kuliko jengine, basi atalifuata lile lenye uzito kwake, kisha aikamilishe swala yake kulingana na hilo (lenye uzito), kisha atoe salamau, asujudu (sujood as-Sahw) na hatimae atoe tena salamu. Mfano wake ni iwapo mtu ameswali swala ya Adhuhuri na akashuku katika rakaa'ah (kama emma ni) ya pili au ya tatu? lakini iliyo na uzito katika fahamu yake ni kwamba hiyo ni rakaa'ah ya tatu, kwahivyo ataifanya kuwa ni ya tatu. Basi baada ya kuitekeleza rakaa'ah moja zaidi, atatoa salamu, asujudu (sujood as-Sahw) na hatimae atoe tena salamu. Ushahidi huu umethibitishwa kwenye Saheeh mbili na kwengineko kutoka katika hadeeth ya 'Abdullaah ibn Mas'ood (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema:

"Awapo na shaka mmoja wenu katika swala yake, basi ajitahidi kulifikilia lililo sawa na aikamilishe juu ya msingi huwo. Kisha na atoe salaam atekeleze sijda mbili."

Hayo ni maneno yalonukuliwa kutoka kwa al-Bukhaaree.

(ii) Njia zote mbili za uwezekano hazina uzito katika fahamu yake. Kwahivyo itambidi alitekeleze lile alilo na hakika nalo, ambalo litakuwa ni lenye uchache miongoni mwa mambo mawili, kisha aikamilishe swala yake juu ya msingi huwo, kisha asujudu (sujood as-Sahw) **kabla** ya kutoa salaam.

Mfano wa hayo ni iwapo mtu ameswali

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

swala ya 'Asr na akawa na shaka katika rakaa'ah (iwapo hiyo) ni ya pili au ya tatu na hizo zote zisiwe na uzito wowote katika fahamu yake.
Kwahivyo ataifanya hiyo kuwa ni ya pili, atekeleze tashah-hud ya kwanza na rakaa'ah mbili baada ya hapo na kisha asujudu (sujood as-Sahw) na hatimae atoe salamu.
Ushahidi huu umetokana na riwaya iliyopokewa na Muslim kutoka kwa Aboo Sa'eed al-Khudhree' (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema:
"Atakapokuwa na shaka mmoja wenu katika swala yake na asijue ameswali (rakaa'ah) ngapi - iwapo ni rakaa'ah tatu au nne - basi na aitupilie mbali shaka na aanze pale alipo na hakika napo. Kisha na atekeleze sijda mbili kabla ya kutoa salaam. Kwahivyo ikiwa ameswali (rakaa'ah) tano, hiyo itamkamilishia swala yake, na ikiwa ameziswali nne kamili, basi utakuwa huwo ni utwevu (tahayuri) kwa shetani."
Na ni katika miongoni mwa mifano ya shaka awapo mtu amewasili na Imaam akawa kwenye rukoo'. Akaitamka (takbeeratul-Ihraam) takbeer ya mwanzo akiwa amesimama wima na kisha akarukoo', matokeo yake hapo yatakuwa ni miongoni mwa mambo matatu:
(i) Mtu huyu alikuwa na hakika yakwamba alipowasili alimkuta Imaam kwenye rukoo' kabla hajainuka. Kwahivyo hapo ameipata rakaa'ah hiyo na hahitajiki kuisoma Sooratil-Faatihah katika hali hii;
(ii) Mtu huyu alikuwa na hakika yakwamba Imaam ameshainuka kutoka kwenye rukoo' kabla yeye hajamfikia, basi itakuwa rakaa'ah hiyo imemkwepa (ameikosa).
(iii) Akawa na shaka kuhusu kuwasili kwake kwa Imaam alipokuwa amerukoo' ili nae awe ameipata rukoo'hiyo; au iwapo Imaam aliinuka kutoka kwenye rukoo' kabla hajampata ili nae awe ameikosa rakaa'ah hiyo. Sasa iwapo mojawapo itakuwa na uzani katika fahamu yake, basi atatekeleza juu ya hayo na akamilishe swala yake juu ya msingi huo na atoe salaam, atekeleze sijda ya kusahau na kisha atoe salaam.
Hali hii ni iwapo hakukosa chochote kwenye swala kwa sababu haitompasa kusujudu katika hali hiyo. Lakini ikiwa hali zote hizo mbili hazina uzito wowote kwenye fahamu yake basi atatekeleza juu ya yale alonahakika nayo (ambayo ni; ameikosa rakaa'ah), kwahivyo atakamilisha swala yake juu ya msingi huwo na atasujudu kwa kusahau **kabla** ya kutoa salaam, kisha atoe salaam.
(Fahamu): Akiwa na shaka katika swala yake atafuata lile alilo na hakika nalo, au lile alilo na uzito zaidi kwenye fahamu yake. Kulingana na yaliyokwisha tajwa hapo mbeleni. Kisha itakapo-mdhihirikia yakwamba kitendo alichokitanguliza kimeandamana kulingana na uhakika, ambao ni hakuongeza wala hakupunguza chochote katika swala yake, basi haitompasa kuitekeleza sijda ya kusahau. Kulingana na inavyofahamika kutoka kwenye madh-hab, hayo ni kwa sababu ile shaka iliyoshurutisha haipo kamwe. Kinyume cha hivyo, inasemekana ni sharuti lifanywe jambo hilo ili kumtahayarisha Shetani, kwa kutokana na maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم):
"Na iwapo aliiswali (swala yake) kikamilifu basi hizo sijda mbili zitakuwa ni tahayuri kwa Shetani."
Na kutokana na sababu yakwamba aliiswali sehemu ya swala yake katika hali ya shaka kulingana na utekelezaji wake, na huu ndiwo msimamo ulosihi zaidi.
Mfano wake (ni iwapo) mtu ameswali na akawa na shaka kwenye rakaa`ah emma ni rakaa`ah ya pili au ya tatu. Na uwezekano baina ya tafauti mbili hizi usiwe na uzito kwenye fahamu yake, basi akaifanya kuwa ni rakaa`ah ya pili na akakamilisha swala yake juu ya msingi huo. Lakini alipokuwa akiendelea (na swala yake) ikadhihirika kwake yeye yakwamba kwa hakika ilikuwa ni rakaa`ah ya pili. Katika hali hiyo, haitompasa yeye kutekeleza sijda ya kusahau kulingana na umaarufu katika madh-hab, lakini kusujudu kwa ajili ya kusahau **kabla** ya salaam kunahitajika kutoka kwake na haya mapendekezo ya pili ndiyo tuliyosimama nayo.

KUSUJUDU KWA AJILI YA KUSAHAU KWA YULE ANAESWALI NYUMA YA IMAAM:

Ikiwa Imaam amesahau basi ni waajib juu ya wale wanaomfuata kwenye swala wamfuate katika kuitekeleza sijda ya kusahau kutokana na maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم):
"Imaam amewekwa afuatwe, kwahivyo musikhalifiane nae..."
mpaka aliposema,
"... anaposujudu basi nanyi musujudu..."
Wameafikiana juu ya hadeeth hii kutoka katika hadeeth ya Abu Hurairah (رضي الله عنه). Kwahivyo, emma Imaam amesujudu kwa kusahau kabla ya salaam au baada yake, watawajibika pia wale walio nyuma yake. Watafanya hivyo hapo, isipokuwa kwa yule aliewasili kwa kuchelewa na akataka kukamilisha sehemu ya swala aliyoikosa; mtu huyu hatomfuata Imaam katika kuitekeleza sijda baada ya salaam, kwani hapana uwezekano kwake kufanya hivyo. Hii ni kwasababu hawezi yeye kutoa salaam pamoja na Imaam, kwahivyo linalompasa yeye mwanzo ni kukamilisha alichokikosa, na kisha atoe salaam, kisha asujudu kwa kusahau, na hatimae atoe salaam.
Mfano wake (ni iwapo) mtu amejiunga na swala pamoja na Imaam katika rakaa'ah ya mwisho, na Imaam ikampasa kusujudu kwa ajili ya kusahau baada ya kutoa salaam. Sasa Imaam atakapotoa salaam, mtu huyu atasimama ili akamilishe alichokikosa na wala asisujudu pamoja na Imaam.
Akisha kukamilisha alichokikosa na akatoa salaam, itampasa atekeleze sijda ya kusahau baada ya kutoa salaam hii. Lakini iwapo mfuasi (ma'moomah) na sio Imaam amesahau katika swala yake, na akaipata swala yote kamili, basi haitompasa kusujudu (sujood as-Sahw). Hii ni kwa sababu kusujudu kwake kutamfanya amukhalifu Imaam na aiharibu ile hali ya kumfuata Imaam.
Vilevile, Maswahaba nao (رضي الله عنهm) waliiacha tashah-hud wakati Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipoisahau, kwahivyo walisimama pamoja nae na hawakukaa kwa tashah-hud ili watekeleze kwa mujibu wa kumfuata wala sio kumukhalifu Imaam.
Lakini ikiwa amekosa sehemu ya swala kutokana na kusahau hali yakuwa anaswali nyuma ya Imaam, au alipokuwa akikamilisha alichokikosa akiwa peke yake, basi itambidi asujudu kwa ajili ya kusahau baada ya kukamilisha alichokikosa. Sijda hii itakuwa ni emma kabla au baada ya kutoa salaam, itategemea sababu zake, kama ilivyotangulia hapo awali.
Mfano wake (ni iwapo) mfuasi amesahau kusema,"Subhaana rabbiyal-Adheem" kwenye rukoo', lakini hakukosa kitendo chochote cha swala, haitompasa kusujudu. Lakini akikosa rakaa'ah au zaidi, basi ni lazima aikamilishe na kisha asujudu kwa kusahau kabla ya salaam.
Mfano mwengine (ni iwapo) mfuasi ameswali swala ya adhuhuri pamoja na Imaam, kisha Imaam aliposimama kwa rakaa'ah ya nne, mfuasi akabakia chini amekaa akidhania yakwamba hiyo ni rakaa'ah ya mwisho. Lakini alipojua yakuwa Imaam ameshasimama nae

akasimama. Kwahivyo ikiwa hakukosa chochote katika swala basi hatopaswa kusujudu. Lakini kitendo hicho kikimsababisha yeye aikose rakaa'ah au zaidi basi itambidi akamilishe alichokikosa kisha atoe salaam, kisha asujudu kwa kusahau na kisha atoe salaam. Sijda hii ni kwa ajili ya kikao ambacho alichokiongeza katika swala wakati Imaam aliposimama kwa rakaa'ah ya nne.

(FAHAMU): Kutokamana na yaliyotangulia, itadhihiri yakwamba sijda ya kusahau wakati mwengine hutekelezwa kabla ya salaam na wakati mwengine hutekelezwa baada yake. Kwahivyo, hutekelezwa kabla ya salaam ikiwa ni katika hali mbili:
(i) Huwenda ikawa ni kwa ajili ya upungufu, kutokana na hadeeth ya 'Abdullaah ibn Buhaynah (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisujudu kwa kusahau **kabla** ya salaam na alipoacha tashah-hud yakwanza, na hadeeth hiyo imeshatangulia.
(ii) Huwenda ikawa ni kwa ajili ya shaka na akawa hawezi kupambanua baina ya njia mbili za uwezekano, iliyo na uzani kwenye fahamu yake, kutokana na hadeeth ya Abu Sa'eed al-Khudhree (رضي الله عنه) kuhusu atakaekuwa na shaka katika swala yake na asijue ameswali ngapi, emma ni rakaa'ah tatu au nne. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamuamuru mtu huyo atekeleze sijda mbili **kabla** ya salaam, na hadeeth hiyo imeshatangulia. Na sijda ya kusahau hutekelezwa baada ya salaam:
(i) Ikiwa ni kwa ajili ya nyongeza katika swala, kutokana na hadeeth ya 'Abdullaah ibn Mas'ood (رضي الله عنه) wakati Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliposwali swala ya adhuhuri rakaa'ah tano, nao wakampasha habari baada ya kutoa salaam, nae Mtume (صلى الله عليه وسلم) akazitekeleza sijda mbili na kisha akatoa salaam. Wala yeye Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwafafanuliya yakwamba sijda hiyo baada ya salaam ni kwa vile alijua nyongeza hiyo baada yakwamba ameshatekeleza jambo hilo. Kwahivyo hii yaonyesha yakwamba hukmu hii ni kwa ujumla na sijda kwa sababu ya nyongeza hutekelezwa baada ya salaam - iwapo atajua kuhusu nyongeza hiyo kabla ya salaam au baada yake.
Katika hali hii vilevile, hupatikana mtu atoae salaam kwa kughafilika kabla ya kuikamilisha swala yake, kisha akakumbuka na kuikamilisha. Huyu ameongeza salaam ndani ya swala, kwahivyo anastahili kusujudu baada ya salaam kutokana na hadeeth ya Abu Hurairah (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitoa salaam kwenye swala ya Adhuhuri au Al-'Asr baada ya rakaa'ah mbili. Wakampasha habari nae akaikamilisha swala na kisha akatoa salaam, kisha akasujudu kwa ajili ya kusahau, na hadeeth hiyo imeshatangulia.
(ii) Huwenda ikawa ni kwa ajili ya kusahau na jambo moja likawa na uzito katika fahamu yake, kutokana na hadeeth ya ibn Mas'ood (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliamrisha kwa yule atakaesahau katika swala yake na ajitahidi kuisahihisha, na kisha aikamilishe swala yake juu ya msingi huwo, kisha na atoe salaam na asujudu, na hadeeth hiyo imeshatangulia.
Na iwapo imetokea yakwamba amesahahu katika hali zote mbili, mojawapo ikahitaji sijda kabla ya salaam na nyengine ikahitaji sijda baada ya salaam; hapo wanazuoni wamesema sijda kabla ya salaam ni yenye kuzidi nguvu, kwahivyo atasujudu **kabla** ya salaam. Kwa mfano mtu akiwa anaswali swala ya adhuhuri na akasimama kwa rakaa'ah ya tatu bila ya kukaa kitako, kwa tashah-hud ya kwanza, kisha akaketi kitako katika rakaa'ah ya tatu akidhania kuwa hiyo ni rakaa'ah ya pili. Mara akakumbuka yakwamba hiyo ni rakaa'ah ya tatu - basi naasimame, aongeze tena rakaa'ah, kisha na asujudu kwa kusahau na hatimae na atoe salaam. Sasa mtu huyu aliiacha tashah-hud ya kwanza, ambayo inahitaji sijda kabla ya salaam, na akaongeza kikao kwenye rakaa'ah ya tatu, ambayo inahitaji sijda baada ya salaam, kwahivyo sijda kabla ya salaam ndiyo iliyo na nguvu zaidi na Allaah (Subhaanahu wata'aalah) yanamuelea.
Kwahivyo namuomba Allaah atupe fahamu njema sisi pamoja na ndugu wote Waislamu kuhusu kitabu chake na Sunnah za Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم) na tuwe ni wenye kuyaandama mafunzo hayo kwa siri na kwa dhahiri, kuhusiana na 'aqeedah, ibaadah na nyenendo. Na Atutakabalie kila la kheri kwani Yeye ni Mwingi wa Rehma na Mwenye Huruma. Na sifa zote njema ni Zake Allaah, Mola wa viumbe vyote, na tunamuomba Allaah amfikilizie amani Mtume wetu Muhammad (صلى الله عليه وسلم) na wafuasi wake wa kweli na Maswahaba zake. Aameen!

HAKI YA KILA MUISLAMU

NA: Ash-Shaikh ‘Abdur-Rahmaan As-Sa’dee

Katika uchambuzi wake wa hadeeth kuhusu haki za Muislamu, amesema ash-Shaikh ‘Abdur-Rahmaan As-Sa’dee: Amesema Abu Hurayrah (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم): **“Haki za Muislamu juu ya Muislamu mwenziwe ni sita.” Maswahaba wakamuuliza, “Na ni zipi Ewe Mjumbe wa Allaah?” Nae akawajibu: “Utakapokutana nae, msalimie kwa maamkuzi ya amani, Atakapokualika, uitikie ualishi wake, Akutakapo nasaha, mnasihi, Atakapochemua na akasema Alhamdulillaah, muitikie kwa kumwambia Yarhamukallaah, Awapo mgonjwa, nenda ukamzuru, na atakapokufa, mfuate (yaani; nenda ukamzike).”** Hadeeth hii imepokewa na Imaam Muslim.
Yoyote mwenye kuzitekeleza haki hizi sita, juu ya Muislamu mwenzake, basi ajue yakwamba kuyatekeleza mambo mengine (mbali na yaliyo wajibu juu yake) ni aula zaidi. Na katika kumtekelezea Muislamu mwenziwe mambo haya kunamfanya yeye mwenyewe kuwa ni mwenye kuyatekeleza yampasayo, ambayo ndani yake kuna kheri nyingi na malipo makubwa kutoka kwa Allaah.
HAKI YA KWANZA: Utakapokutana nae, msalimie kwa maamkuzi ya amani.” Kwa hakika maamkuzi ya amani ni sababu ya kujenga mapenzi, ambayo ndiyo yenye kuleta Imani, ambayo ndiyo yenye kumfanya mtu akaingie Peponi. Hii ni kama alivyosema Mtume (صلى الله عليه وسلم), “Naapa kwa Yule ambaye roho yangu iko kwenye Mkono wake, nyinyi nyote hamutoingia Peponi mpaka Muamini, na hamutoamini mpaka mupendane. Jee, nisiwaelekeze kunako mambo ambayo lau mutayafanya, mutakuwa ni wenye kupendana? Peaneni salamu baina yenu.” Maamkuzi ya amani ni katika tabia njema za Uislamu. Kwani kwa hakika katika kila watu wawili wanaokutana huwa wanaombeana baina yao kusalimika na maovu, na rehma, na baraka zenye kuleta kila kheri. Na lenye kufuata ni kwamba uso mteshiteshi na maneno mazuri ya maamkuzi yenye kusababisha umoja na mapenzi, na huondoa hisiya za chuki na kujitenga na watu. Kwahiyo, kutoa salamu za amani ni haki ya Muislamu, na ni wajibu wa mwenye kuamkuliwa kurudisha salamu kama alivyopewa au salamu zenye maamkuzi ya ziada. Na wabora wa watu ni wale wenye kuanza maamkuzi ya salamu kwanza.”
[ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO]